



VIWANDA

Baraza la Mawaziri laidhinisha ruzuku ya Sh117B kwa viwanda vya sukari vinavyomilikiwa na serikal UK 3



UHIFADHI

Wadau katika Kajiado wahimiza sheria za kudhibiti uzoaji wa changarawe UK 7

KILIMO

Wakulima wenye mashamba madogo wataka serikali kulinda sekta ya mbegu za kiasili

MyGov.

www.mygov.go.ke

OKTOBA 17, 2023

TATHMINI YAKO YA WIKI



UK 14

TOLEO No. 16/2023-2024

Idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ualimu yaongezeka pakubwa

Kubadilishwa kwa hitaji la kujiunga na vyuo vya mafunzo ya ualimu ni sehemu ya mapendekezo ya Kamati ya Rais kuhusu Marekebisho ya Elimu (PWPER)



NA DOUGLAS NAMUNANE (PCO)

Takriban wanafunzi 12,000 wamejiunga na Vyuo 32 vya Ualimu vya Umma (TTCs) hivi karibuni kufuatia uamuzi wa Serikali wa kubadilisha masharti ya kujiunga ya wanaotuma maombi mapya.

Mabadiliko haya yameongeza jumla ya idadi ya wafunzi katika vyuo vya mafunzo ya ualimu hadi zaidi ya 14,000, na kuibua maisha mapya katika taasisi hizi, ambazo zimekuwa na shida ya kuwa

Najitolea kutekeleza mapendekezo yote yaliyofanywa na Jopokazi la Rais kuhusu Marekebisho ya Elimu

wanafunzi wachache kwa miaka mingi.

Waziri la Elimu, Ezekiel Machogu, alibainisha kuwa kubadilishwa kwa masharti kumewapa afueni walimu

wengi wanaotarajia kupata mafunzo ya ualimu.

Machogu alisema, "Idadi inaongezeka. Zaidi ya wanafunzi 12,000 wamejiunga na TTC zetu 32, ongezeko kubwa kutoka idadi ndogo ya awali ya 1,700. Hii inaashiria kwamba kwa namna fulani tulikuwa tunakaribia kufunga vyuo vya ualimu."

Kubadilishwa kwa mahitaji ya kujiunga na vyuo vya mafunzo ya ualimu ni sehemu ya mapendekezo ambayo yalipendekezwa na Kamati ya Rais kuhusu Uboreshaji wa Elimu (PWPER).

Katika ripoti yake, timu iliyoongoza na Prof Raphael Munavu iligundua kuwa baadhi ya wenye Cheti cha Elimu ya Sekondari nchini

ENDELEA UK 2

	9 Idadi ya kreni zinazobeba kontena tupu KPA imeongeza kusughulikia idadi kubwa ya mizigo katika bandari ya Kilindini	117B Kiasi cha pesa baraza la mawaziri limeidhinisha kusaidia viwanda sita vya miwa vinavyomilikiwa na serikali maeneo ya magharibi na Nyanza.	Sh2.4B Gharama ya feri ya MV Uhuru II iliyozinduliwa katika Kenya Shipyards Limited (KSL) katika kaunti ya Kisumu.	Sh 25M Gharama ya kituo cha kisasa cha matibabu ya macho kilichoingwa na kaunti ya Taita Taveta katika Moi Referral Hospital, Voi	13,000 Kiasi cha pesa wazoaji changarawe hulipwa kwa kila gari katika kaunti ya Kajiado
--	---	--	--	---	---



Rais William Ruto akiondoka katika meli ya MV Uhuru II cargo ship baada ya kuizindua katika Kenya Shipyards Limited (KSL), kaunti ya Kisumu. Picha na Chris Mahandara

Uwezo wa bandari ya Kisumu waongezeka meli ya MV Uhuru II ikizinduliwa

NA ROBERT OJWANG (KNA)

Kenya iko mbioni kuwa kitovu muhimu cha meli kufuatia kuzinduliwa kwa feri ya kubebea mizigo ya MV Uhuru II, mradi wa thamani ya Sh2.4 bilioni, katika Kampuni ya Kenya Shipyards Limited (KSL) katika Kaunti ya Kisumu.

Wakati wa hafla ya uzinduzi, Rais William Ruto aliangazia umuhimu wa kujengwa meli hii ya urefu wa mita 100, MV Uhuru II, inayosaidia MV Uhuru I na kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya usafirishaji wa bidhaa ndani ya eneo la Ziwa Victoria. Rais aliipongeza KSL kwa kufikia hatua hii muhimu, akisema kwamba inaweka Kenya kama kivutio cha ujenzi na ukarabati wa meli katika eneo la Afrika

Mashariki.

Zaidi ya hayo, alisisitiza uwezo wa Kenya Shipyards kujenga, ukarabati na kudumisha meli kwa ajili ya soko la ndani na kikanda kama ishara ya kujitolea kwa taifa kutumia rasilimali zilizo na vipaji ili kukidhi mahitaji ya kanda ya huduma bora za baharini.

"MV Uhuru II iliyo mbele yetu sio tu chombo cha usafiri, bali pia ni chombo cha kuharakisha ukuaji wa uchumi na maendeleo katika eneo letu. Itarahisisha biashara, kuunda nafasi za kazi, na kufungua fursa kwa biashara kustawi," alisema kiongozi wa nchi.

Dkt Ruto aliongeza, "Kuna

ENDELEA UK 2

Idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ualimu yaongezeka pakubwa

ENDELEA KUTOKA UK 1

Kenya ambao walikuwa wamefikia daraja la wastani la C hawakuweza kupata nafasi ya kujiunga na vyuo mbalimbali vya ualimu kutokana na mahitaji ya makundi mbalimbali.

Machogu, hata hivyo, aliharakisha kusema kuondolewa kwa mahitaji hakukusudiwa kuathiri ubora wa elimu.

"Kilichofanyika hapo awali kilikuwa kukosa hisia, kutowajibika na kwa kweli hatuwezi kuruhusu hali ya aina hiyo. Na ndio maana najitolea kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Utendaji ya Rais na kuondoa kipengele kilichokuwepo hapo awali ambacho haimaanishi kuwa tunahatarisha ubora wa elimu," alisema.

Machogu aliyasema hayo katika kaunti ya Mandera wakati akiwaongoza maafisa wengine wa elimu kuzindua miradi mbalimbali ya miundombinu ikiwemo Chuo cha Ualimu cha Mandera, Taasisi ya Mafunzo ya Ufundi pamoja

na Ripoti ya Jopo la Elimu la kaunti.

Alisema serikali itatekeleza kwa ujumla mapendekezo katika ripoti ya PWPER.

Wakati huo huo, waziri alipiga marufuku uhamisho wa walimu wasio wenyeji kutoka Kaunti za Kaskazini mwa Kenya.

"Tabia hii ya baadhi ya watu kusema kwamba wanataka kuhama eneo hili kwa sababu moja au nyingine, hatutakubali wala kukubaliana nayo," aliongeza.

Bw Machogu aliendelea kusema kuwa, serikali imejipanga kukabiliana na uhaba wa walimu katika kaunti za kaskazini mwa nchi.

"Tutachukua hatua kwa kuhakikisha kwamba tunasajili walimu zaidi sasa

katika vyuo vyetu vya ualimu," waziri aliongeza. Alisema kwamba serikali imeweka mikakati kuhakikisha mitihani haipatikani kabla ya wakati wa kuifanya kote nchini.

Uwezo wa bandari ya Kisumu waongezeka meli ya MV Uhuru II ikizinduliwa

ENDELEA KUTOKA UK 1

matarajio makubwa ya kibiashara katika ujenzi, ukarabati na utengenezaji wa meli za baharini katika eneo hili na ninaomba KSL kutafuta fursa hizi."

Rais Ruto alidokeza kuwa Kenya Shipyards imepewa kandarasi ya kukarabati na kutunza meli za baharini za wizara mbalimbali, idara za serikali, na mashirika kama vile Mamlaka ya Bandari ya Kenya, Walinzi wa Pwani ya Kenya, Mamlaka ya Bahari ya Kenya, Taasisi ya Utafiti wa Bahari ya Kenya na waendeshaji wengine wa kibinafi katika Bahari Hindi na Ziwa Victoria.

Kulingana na Rais, ufufuzi wa sekta ya usafiri wa baharini na usafirishaji Kenya kupitia ujenzi

Kuna nafasi nyingi za kazi katika ujenzi, ukarabati wa vifaa vya usafiri baharini "Rais



Meli iliyogharimu Sh2.4Billioni MV Uhuru II iliyozinduliwa na Rais William Ruto katika Kenya Shipyards Limited (KSL) kaunti ya Kisumu. Picha na Chris Mahandara

wa meli unalanda na Ajenda ya Mabadiliko ya Kiuchumi ya kuanzia mashinani (BETA) ambayo inatambua uchumi wa baharini kama sehemu muhimu ya ukuaji endevu wa uchumi wa kitaifa. Akizungumza katika

hafla hiyo hiyo, Mkurugenzi Mkuu, KSL, Meja Jenerali Paul Otieno alibainisha kuwa MV Uhuru II ambayo ilijengwa kutoka mwanzo na wafanyakazi wa KSL kwa ushirikiano na kampuni ya Damen Gorinchem kutoka

Uholanzi ingeongeza uwezo wa bandari ya Kisumu hadi zaidi ya tani 2,300.

Meli hiyo, alisema, itasafiri, kuunganisha uchumi, kuunda ushirikiano na kuchangia biashara ya baharini ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.



MWALIKO WA TENDA

Retirement Benefits Authority ilianzishwa 1997 kupitia Sheria ya Bunge ili kusimamia, kuangalia, na kukuza mifumo ya mafao ya kustaafu, na kukuza sekta ya mafao ya kustaafu.

Mamlaka inakaribisha zabuni zilizofungwa kutoka kwa wabunifu wanaostahili kwa yafuatayo

Nambari ya Tenda	Maelezo ya Tenda	Wastahiki	Tarehe ya mwisho
RBA/OT/GENINS/613/1749/2023	Utoaji wa Bima ya Kikundi ya Jumla	Open	Oktoba 26, 2023 saa 11:00 asubuhi

Nyaraka za zabuni na maelezo yanaweza kupatikana kutoka Ofisi ya Retirement Benefits Authority, Rahimtulla Tower, ghorofa ya 14, Barabara ya Upper Hill, Nairobi, kwa malipo yasiyorejeshwa ya Ksh. 1,000.00. Fedha hizo lazima ziwekwe kwenye akaunti ya KCB ya RBA namba 110 327 5119, Tawi la Milimani. Pia, unaweza kupakua nyaraka za zabuni bila malipo kutoka kwenye wavuti ya RBA - www.rba.go.ke au kutoka kwenye Portal ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma (PPIP) kwenye www.ppip.go.ke. Nyaraka zote za zabuni lazima ziwe wazi kabisa na kuandikwa na nambari ya kumbukumbu ya zabuni husika, na maelezo ya zabuni kisha zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji, Mamlaka ya Faida za Uzee, Rahimtulla Tower, Barabara ya Upper Hill, S.L.B. 57733-00200 Nairobi. Tenders zote zilizokamilika kwa mujibu lazima ziwekwe kwenye Sanduku la Zabuni kwenye Ghorofa ya 14, Rahimtulla Tower, Barabara ya Upper Hill, Nairobi, kabla ya tarehe iliyotajwa. Zabuni zitafunguliwa mbele ya wazabuni au wawakilishi wao ikiwa watapenda kuhudhuria.

Kwa maswali kuhusu Sekta ya Faida za Uzee au mpango wako wa pensheni, tafadhali piga simu kwa RBA bila gharama kupitia namba: 0800720300.

Kwa taarifa zaidi, tufuate kwenye



Retirement Benefits Authority (RBA) is ISO 9001: 2015 Certified



PUBLIC NOTICE

PUBLIC PARTICIPATION FORUMS ON PROPOSED POLICY CHANGES TO THE RETIREMENT BENEFITS ACT AND REGULATIONS

Retirement Benefits Authority was established under the Retirement Benefits Act, Cap 197 No. 3 of 1997 to regulate and supervise establishment and management of retirement benefits schemes; protect the interest of members and sponsors of retirement benefits schemes; approve trustees' remuneration approved by members during the annual general meeting after every three years; promote development of the retirement benefits sector; and, advise the Cabinet Secretary of The National Treasury on the national policy to be followed with regard to the retirement benefits sector.

In line with the Statutory Instruments Act No. 23 of 2013 and Article 118 of the Constitution on consultation before making statutory changes, the Retirement Benefits Authority wishes to invite the public particularly, the stakeholders in the Retirement Benefits sector on the proposed policy changes during public stakeholders' engagement forums in various towns as per the schedule below.

TOWN	VENUE	DATE
Nairobi	Mercure Hotel	6 th November 2023
Mombasa	Voyager Beach Resort	30 th October 2023
Kisumu	The Vic Hotel	30 th October 2023
Kakamega	Golf Hotel Kakamega	31 st October 2023
Eldoret	Eka Hotel	2 nd November 2023
Machakos	Machakos University	1 st November 2023
Nyeri	The White Rhino Hotel	1 st November 2023
Meru	Three Steers Hotel	2 nd November 2023
Nakuru	The Alps Hotel	30 th October 2023

The draft policy changes can be downloaded from the Authority's website (www.rba.go.ke). All meetings are scheduled to take place from 8:30 am to 5:00 pm. Members of the public and interested stakeholders are invited to participate and confirm participation or send their written memorandum through research@rba.go.ke on or before **27th October 2023**.

RETIREMENT BENEFITS AUTHORITY
Rahimtulla Tower, 13th Floor, Upper Hill Road, P.O. Box 57733-00200 Nairobi
Tel: 2809000 Mobile: 0726600001-5 or 0735339132 Fax: 2710330
Email: info@rba.go.ke Website: www.rba.go.ke

Retirement Benefits Authority (RBA) is ISO 9001: 2015 Certified

Baraza la Mawaziri laidhinisha ruzuku ya Sh117b kwa viwanda vya sukari

NA CHRIS MAHANDARA (KNA)

Baraza la mawaziri limeidhinisha Sh117 bilioni kuokoa viwanda sita vya sukari vinavyomilikiwa na serikali katika eneo la Magharibi na Nyanza.

Wakati wa kikao kilichofanyika katika ikulu ndogo la Kisumu, Baraza la Mawaziri liliagiza Hazina ya Kitaifa kutayarisha stakabadhi zinazohitajika ili kuwezesha mchakato huo.

Rais Dkt William Ruto, ambaye aliongoza mkutano huo alisema, serikali itawasilisha bajeti ya ziada kwa Bunge la Kitaifa ili kuidhinishwa ili fedha hizo zipatikane huku serikali ikielekea kufufua sekta ya sukari.

“Baraza la Mawaziri limeidhinisha Sh117 bilioni ili kufuta madeni ya kampuni sukari sita za sukari za serikali. Hii itahakikisha kuwa madeni haya yote yameondolewa tunapoelekea kukodisha viwanda vya sukari,” akasema.



Rais William Ruto na Mkurugenzi Mkuu wa, Kenya Shipyards Limited Meja Jenerali Paul Otieno wakati wa uzinduzi wa meli ya MV Uhuru II katika Kenya Shipyards Limited (KSL), Kisumu. Picha na Chris Mahandara

Akizungumza katika kampuni ya Kenya Shipyards Limited (KSL) mjini Kisumu, ambapo alianzisha meli mpya ya MV Uhuru II, rais alisema uokoaji

Eneo hili lina uwezo wa kuzalisha mimea mingine kama pamba na mahindi-Rais

huo unalenga kampuni za Sukari za Nyanza Kusini (SONY), Nzoia Muhoroni, Chemelil, Miwani na Mumias ambazo ni zilizotengwa kukodishwa.

Serikali, alisema, imedhamiria kufufua sekta hiyo na kuongeza kuwa pesa hizo zitatolewa kwa viwanda kufikia wiki hii huku maandalizi ya kukodisha kampuni zikiendelea.

Kukodisha, aliongeza, kuliwekwa ili kuingiza

mtaji katika kampuni zinazohangaika na kuhakikisha zinafanya kazi kikamilifu ili kuokoa wakulima. Mpango huo alisema umepangwa kuwanufaisha wakulima na hata jamii na kuongeza kuwa ardhi ambayo viwanda hivyo vimejengwa itaendelea kuwa mikononi mwa jamii na serikali. Jamii sasa itatumia serikali ya kaunti au shirika watakalokubali kunufaika kutoka ardhi inayomilikiwa na viwanda,” alisema.

Kando na miwa, alisema serikali kupitia Mpango wa Mabadiliko ya Kiuchumi ya kuanzia mashinani (BETA) iko mbioni kufufua kilimo katika eneo la Nyanza.

“Siyu miwa pekee ambayo tunaangazia. Eneo hili lina uwezo wa kuzalisha mazao mengine mengi yakiwemo pamba, mahindi, mboga na maharagwe,” alisema. Miongoni mwa afua muhimu, alisema ni upanuzi wa Mradi wa Unyunyuzaji wa Lower Nzoia kwa gharama ya Sh5.9 bilioni. Uwekezaji huo, alisema, utawezesha mpango huo kupanuliwa kwa ekari 20,000 zaidi.

Mradi sawa na huo, aliongeza, umepangwa katika Kaunti ya Migori huku Mradi wa Unyunyuzaji wa Kuja ukipangwa kupanuliwa kwa ekari 14,000.

ADC yajitolea kuleta utoshelevu wa chakula kupitia ushirikiano

NA SADIK HASSAN(KNA)

Bodi mpya ya Shirika la Maendeleo ya Kilimo (ADC) iliyozinduliwa hivi majuzi imejitolea kuhakikisha kuwa nchi inajitosheleza kwa chakula kufuatia ukame wa muda mrefu.

Ili kufikia lengo hili, Bodi inatafuta kikamilifu ushirikiano na sekta ya kibinafsi, ikilenga kuongeza uwezo wa ardhi ya ADC katika Galana Kulalu, Kaunti ya Tana River, na ADC Kisiwani Complex huko Malindi, Kaunti ya Kilifi.

Mohammed Bulle, Mkurugenzi Mkuu wa ADC, alihimiza ushirikiano wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kupitia Sheria ya PPP, na nia ya ADC kufuata mwelekeo huo.

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea jengo la ADC Kisiwani Complex lililopo Malindi, ambapo Bodi hiyo mpya ikiongozwa na Mwenyekiti Abdillahi Alawy, ilitembelea mradi wa Galana

Kulalu uliopo Tana River, Bulle alieleza dhamira ya Bodi hiyo ya kutafuta washirika wanaofaa wa sekta ya kibinafsi ili kuimarisha uzalishaji wa chakula na utoshelevu wa lishe ndani ya nchi.

Mashirika kadhaa ya sekta ya kibinafsi yakiwemo Nyumba Foundation, Twiga Foods, na Sheldrick Wildlife Trust, yamewasilisha maombi ya kutaka kushirikiana na serikali.

Ushirikiano huu unalenga kukuza uzalishaji wa ndani wa mafuta ya kula, kuongeza uzalishaji wa mahindi, na kuchangia katika juhudi za kuhifadhi wanyamapori na mimea katika eneo la Shamba la Galana.

Bodi imetembelea maeneo mengine ya nchi ikiwa ni pamoja na Kitale, ambako kuna vituo vya sate-laiti vya ADC.

Kulingana na Mkurugenzi Mkuu, ushirikiano na sekta ya kibinafsi, utafanyika Galana na sio katika eneo la ADC Kisiwani.



SHAHADA YA HESHIMA



HON. DALMAS OTIENO ANYANGO, EBS, EGH.

DALMAS OTIENO ANYANGO, EBS, EGH, WAZIRI WA ZAMANI WA MIPANGO NA AJIRA, WAZIRI WA ZAMANI WA UCHUKUZI NA MAWASILIANO, NA WAZIRI WA ZAMANI WA VIWANDA NA WAZIRI WA HUDUMA ZA UMMA NA MBUNGE WA ENEO BUNGE LA RONGO

Kwa kuzingatia vifungu vya Sehemu ya 7, (1) (c) ya Cheti cha Rongo (2016) na Sheria XXIX ya Rongo Chuo Kikuu, Baraza la Chuo Kikuu la Rongo na Seneti inateuwa Bw. Dalmas Otieno Anyango kwa ajili ya kutoa Shahada ya Heshima ya Daktari wa Sanaa (Hon. D. Arts) ya Chuo Kikuu cha Rongo wakati wa Sherehe ya 8 ya Mahafali itakayofanyika Alhamisi, tarehe 19 Oktoba 2023.

Uteuzi wa Bw. Dalmas Otieno ni kwa kutambua mafanikio yake makubwa katika kuendeleza elimu nchini kupitia miradi kama vile kutoa ufadhili kamili kwa wanafunzi wenye mahitaji, mafanikio yake katika utumishi wa kibinafsi na wa umma, na mchango wake katika utawala, maadili ya kitaifa, na maendeleo.

Chuo Kikuu cha Rongo kinakaribisha Wakenya na jumuiya ya kimataifa kujumuika nasi katika kusherehekea mafanikio ya kipekee ya Bw. Dalmas Otieno Anyango kwa kuboresha jamii.

Prof. Samuel Gudu
NAIBU CHANSELA



MINISTRY GENDER, CULTURE, THE ARTS AND HERITAGE

STATE DEPARTMENT FOR CULTURE, THE ARTS AND HERITAGE

NAKALA YA OMBI LA PENDEKEZO LA HUDUMA ZA USHAURI

Tunakaribisha tenda kutoka kwa wakandarasi wote wanaostahili kutekeleza huduma zifuatazo: -

ITEM	NAMBARI YA TENDA	MAELEZO	ADA YA TENDA	DHAMANA	TAREHE YA MWISHO
1.	SDFH/RFP/ONT/02/2023/2024	Ombi la pendekazo la kutoa huduma za ushauri	Pakua bila malipo kutoka kwa mtandao wa PPIP www.tenders.go.ke .	280,000.00	24 th October, 2023

Wazabuni wote walio na nia na waliosajiliwa katika sekta na vitengo vinavyofaa, (uthibitisho wa usajili unahitajika) Wanaweza kupakua Nyaraka za Tenda kutoka wavuti ya PPIP bila malipo.

Wazabuni wenye nia wanapaswa kuzingatia kwamba ni wale tu wanaokidhi vigezo vilivyoinishwa katika nyaraka za tenda, kama kiwango cha chini, na kuambatisha nyaraka zinazofaa wakati wa kuwasilisha, ndio watakapewa kipaumbele katika tathmini.

Tenda zilizowekwa kwenye bahasha na kuandikwa jina na nambari ya tendai kwenye pembe ya kulia ya juu na bila kutoa taarifa yoyote kuhusu mpiga zabuni yanapaswa kutumwa kwa: -

Katibu
Ministry of Gender, Culture The Arts and Heritage
State Department for The Arts, Culture and Heritage
S.L.P 49849 -00100
NAIROBI.

na kuwekwa katika Sanduku la Zabuni ifikapo tarehe 24 Oktoba, 2023 saa 10.00 asubuhi.

Mambo yaliyowasilishwa yatafunguliwa hadharani baada ya tarehe na muda wa kufunga uliotajwa hapo juu, mbele ya washiriki au wawakilishi wao wanaochagua kuhudhuria. Zabuni zilizowasilishwa baada ya muda wa kufunga zitarudishwa zikiwa hazijafunguliwa.

Bei zilizotolewa lazima ziwe halali kwa siku mia ishirini (120) tangu tarehe ya kufunguliwa kwa zabuni.

Mteja anahifadhi haki ya kukataa zabuni yoyote na hauku na wajibu wa kukubali zabuni iliyo chini kabisa au zabuni yoyote.

SCMO



KPA yapanua Bandari ya Mombasa na miundombinu ili kukuza biashara

NA MATHEW CHEKEWEL(MYGOV)

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ya Kenya (KPA) inaweza pakubwa katika miradi mbalimbali ya bandari kote nchini ili kuhakikisha kuwa vifaa vyake vinasalia kuwa na ushindani ndani ya kanda ya Afrika.

Mkurugenzi Mkuu wa KPA, Kapteni William Ruto, ameangazia matukio

muhimu yanayoendelea.

Mombasa, bandari kubwa na yenye shughuli nyingi zaidi katika Afrika Mashariki na Kati, inapangiwa kupanuliwa. Awamu ya pili ya kituo cha pili cha kontena sasa kinafanya kazi, na hivyo kuongeza uwezo wa bandari hiyo kwa mwaka hadi TEU milioni 2.1.

Kreni na vifaa vipya vya

meli hadi ufukweni vimenunuliwa ili kuongeza ufanisi katika kushughulikia mizigo. Ili kukidhi kuongezeka kwa shehena katika Bandari ya Kilindini, KPA imeongeza vidhibiti tisa vya kontena tupu, vibandiko 12 vya kufikia na trekta.

Kreni za kuhamishwa Bandarini zimetumwa katika Bandari ya Lamu. Maendeleo yanayoendelea



Mkurugenzi Mkuu wa KPA Nahodha William Ruto

ya Bandari ya Lamu hivi karibuni yataigeuza kuwa kituo cha kontena chenye uwezo kamili.

Hatua hizi zinatarajiwa kuboresha tija kwa kiasi kikubwa, kupunguza muda wa kushughulikia meli bandarini.

Kufika hivi majuzi wa meli ya shehena kubwa la Shirika la Mpango wa Chakula Duniani katika Bandari ya Lamu kumechochea mashirika ya kiserikali kusaidia maendeleo ya miundombinu ili kuvutia meli zaidi kwenye bandari hiyo

mpya.

KPA inashirikiana na mashirika mbalimbali ya serikali ili kuharakisha ukamilishaji wa miundombinu muhimu kama vile mitandao ya barabara, yadi za udhibiti wa malori, na vituo vya huduma, kuwezesha utiririshaji wa shehena kutoka bandarini. KPA ina nia ya kufungua uwezo wa kibiashara na nchi jirani, kama vile Ethiopia na Sudan Kusini, ambazo ziko tayari kutumia Bandari ya Lamu kwa mauzo ya mifugo na uagizaji wa mbolea.



NOTISI YA TENDA

Geothermal Development Company Limited (GDC) inaika maombi ya tenda kutoka kwa wagembea wanaostahiki kutoa huduma zifuatazo:

NAMBARI YA TENDA	MAELEZO YA TENDA	KUNDI LINALOLENGWA	DHAMANA	TAREHE YA MWISHO
GDC/FIN/OT/019/2023:2024	Zabuni ya Huduma ya Ukaguzi (Uthibitisho wa Matumizi).	Wazi kwa wote	Kshs. 100,000	02/11/2023 at 11:00AM
GDC/DO/OT/020/2023:2024	Zabuni ya Ugavi wa Lubricants kwa Mradi wa Umememvuke wa Baringo Silali.	Wazi kwa wote	Kshs. 200,000	03/11/2023 at 11:00AM
GDC/FLT/OT/022/2023:2024	Zabuni ya Upangishaji wa Magari kwa Kipindi cha Miaka Minne (4).	Wazi kwa wote	Kshs. 1,000,000	15/11/2023 at 11:00AM
GDCSRBS/OT/024/2023:2024	Zabuni ya Huduma za Ukaguzi wa Nje kwa Mfumo wa Malipo ya Uzeeni ya Wafanyakazi wa GDC kwa Mitatu (3).	Wazi kwa wote	Kshs. 100,000	01/11/2023 at 11:00AM
GDC/DEM/OT/025/2023:2024	Zabuni ya Ugavi na Utoaji wa Mfumo wa Taa za Jua kwa Mradi wa Umememvuke wa Baringo Silali.	Vijana walio na Cheti cha AGPO	Fomu ya Azimio la Kujitolea kwa Zabuni iliyojazwa kwa usahihi, iliyo sainiwa na kuwekwa muhuri.	08/11/2023 at 11:00AM
GDC/DEM/OT/026/2023:2024	Zabuni ya Ugavi na Usanikishaji wa Nyaya za Kupandisha kwa Mradi wa Umememvuke wa Baringo Silali.	Wazi kwa wote	Kshs. 200,000	09/11/2023 at 11:00AM
GDC/GRM/OT/027/2023:2024	Zabuni ya Ugavi wa Vifaa vya Kurekodi na Vifaa vya Nyongeza kwa Mradi wa Umememvuke wa Baringo Silali.	Wazi kwa wote	Kshs. 200,000	10/11/2023 at 11:00AM

Kutakuwa na ziara ya lazima kwenye eneo la GDC la Baringo Silali kwa Zabuni ya Upangishaji wa Magari kwa Kipindi cha Miaka Minne (4) - **Namba ya Zabuni: GDC/FLT/OT/022/2023:2024** siku ya Jumatano, tarehe 1 Novemba 2023 saa 10:00 asubuhi katika Mradi wa Umememvuke wa Baringo-Silali. **(Wazabuni wanahitajika kukusanyika katika Ofisi ya GDC Kaskazini Rift Kapkerwa saa 9:30 asubuhi).** Ramani ya Ofisi ya GDC Kapkerwa imeambatanishwa.

Wazabuni wanaostahiki na wenye nia wanaweza kupata habari zaidi na kukagua waraka wa zabuni kutoka kwa Afisa Meneja, Ugavi katika Jengo la Kawi, South C karibu na Barabara ya Mombasa, Barabara ya Msalaba Mwekundu kati ya saa 9 asubuhi na saa 4 alasiri wakati wa siku za waki.

Mkusanyiko kamili wa hati za zabuni unaweza kupatikana na kampuni zenye nia kwa malipo yasiyorejeshwa ya Kshs. 1000 yanayolipwa kwa ofisi yetu kwa pesa taslimu au hundi ya benki. Waraka unaweza pia kuonekana na kupakuliwa kutoka kwenye tovuti www.gdc.co.ke au [PPIP Portal www.tenders.go.ke](http://www.ppipportal.com) bila malipo.

Wazabuni wanaopakua waraka wa zabuni kutoka kwenye tovuti **WANATAKIWA** kutuma taarifa zao mara moja kwa procurement@gdc.co.ke kwa madhumuni ya kuhifadhi rekodi na ufafanuzi wa zabuni na marekebisho mengine yoyote.

Zabuni zilizokamilishwa na kuwekwa ndani ya bahasha tupu iliyofungwa na kuandikwa namba ya Zabuni na jina la kumbukumbu ya Zabuni; zitumwe kwa anwani ifuatayo:

Mkurugenzi Mkuu/Afisa Mkuu Mtendaji,
Geothermal Development Company
S.L.P 100746-00101
NAIROBI, KENYA

na kuziweka kwenye sanduku la zabuni katika Ghorofa ya Chini ya ofisi ya GDC, Kawi House, South C karibu na Barabara ya Mombasa, Barabara ya Msalaba Mwekundu ifikapo tarehe zilizotajwa hapo juu.

Tenda zitafunguliwa mara moja baadaye mbele ya wazabuni au wawakilishi wao wanaochagua kuhudhuria katika Kawi House, South C, GDC Board Room, Ghorofa ya Chini.

Zabuni zilizowasilishwa baada ya muda wa kufunga hazitakubaliwa.

MENEJA, UNUNUZI WA BIDHAA



COMMUNICATIONS
AUTHORITY OF KENYA

NOTISI YA TENDA

Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya ndiyo mamlaka ya udhibiti wa tasnia ya ICT nchini Kenya na majukumu katika mawasiliano ya simu, biashara, utangazaji, na huduma za posta na kourier. CA pia inawajibika kwa usimamizi wa rasilimali za namba na masafa ya nchi na utawala wa Mfuko wa Huduma za Universal (USF) pamoja na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za ICT.

CA inaika zabuni kutoka kwa kampuni zilizo na nia na uwezo wa kutoa huduma zifuatazo:

No	Marejeleo ya Tend	Maelezo ya Tenda	Tarehe ya kufunga na muda wa mwisho	Wanaostahili
1.	CA/SCM/OT/10/2023-2024	Tenda wazi ya Kitaifa ya Ugavi na Utoaji wa UPSs.	Novemba 8, 2023 saa 10:30 asubuhi (Saa ya Afrika Mashariki).	(Imetengewa mashirika ya walemavu)
2.	CA/SCM/OT/11/2023-2024	Tenda Wazi ya Kitaifa ya Ugavi na Utoaji wa Printa za Kazi Nyingi.	Novemba 8, 2023 saa 10:30 asubuhi (Saa ya Afrika Mashariki).	Wazi kwa wote
3.	CA/SCM/OT/12/2023-2024	Tenda wazi ya Kitaifa ya Ugavi na Utoaji wa Vipakatalishi	Novemba 8, 2023 saa 10:30 asubuhi (Saa ya Afrika Mashariki).	(Imetengewa mashirika ya vijana)
4.	CA/SCM/OT/13/2023-2024	Tenda wazi ya Kitaifa ya Ugavi na Utoaji wa Vifaa vya Maabara ya Uchunguzi wa Kidijitali.	Novemba 8, 2023 saa 10:30 asubuhi (Saa ya Afrika Mashariki).	(Imetengewa mashirika ya walemavu)
5.	CA/SCM/OT/14/2023-2024	Tenda wazi ya Kitaifa ya Ugavi, Utoaji, kujenga na kutunza Mfumo wa Usimamizi wa Usalama wa Maktaba.	Novemba 8, 2023 saa 10:30 asubuhi (Saa ya Afrika Mashariki).	Wazi kwa wote

Stakabadhi za zabuni zinaweza kupatikana na kupakuliwa kutoka kwenye Portal ya Taarifa ya Ugavi wa Umma <http://www.tenders.go.ke> na tovuti ya Mamlaka : <https://www.ca.go.ke/open-tenders> bila malipo.

Aidha, kampuni zinazopakua hati ya tenda lazima zitume maelezo yao/taarifa za mawasiliano kwa Meneja wa Usimamizi wa Ugavi, Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya, kupitia anwani ya barua pepe tenders@ca.go.ke kabla ya tarehe ya kufunga kwa madhumuni ya kuhifadhi rekodi na kwa ajili ya kupokea ufafanuzi au marekebisho yoyote, ikiwa yataitokea. Marekebisho yoyote yatakayotolewa yatawekwa kwenye tovuti ya CA.

Washiriki wanaostahiki pia wanaweza kukagua na kupata nakala na maelezo ya kina ya hati ya tendai kutoka Idara ya Ugavi, Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya, kupitia Barabara ya Waiyaki, Nairobi, kati ya saa 9 asubuhi hadi saa 4 alasiri, Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa likizo za umma kwa ada isiyo na marejesho ya Kshs 1,000.00.

Hati za tenda zinaweza pia kupatikana kielektroniki kutoka kwenye Tovuti <https://www.ca.go.ke/open-tenders> au Portal ya Wauzaji ya Taarifa ya Ugavi wa Umma (PPIP) (<http://www.tenders.go.ke/website/tenders/index>). Hati za zabuni uiiyopatikana kielektroniki itakuwa bila malipo.


Bei zilizotajwa zinapaswa kujumuisha kodi zote na LAZIMA zielezwe kwa Shilingi za Kenya.

Hati za zabuni ilyojazwa kwa usahihi inapaswa kuwekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi, iliyofungwa vizuri na kuandikwa kwa wazi jina la zabuni na namba ya kumbukumbu na inapaswa kuwasilishwa kwenye sanduku la zabuni kwenye ghorofa ya chini afisi za CA, ili kufika kabla ya tarehe na muda wa kufunga ulioyeshwa hapo juu.


Director General/CEO
Communications Authority of Kenya (CA)
S.L.P 14448, Nairobi 00800
Simu: +254 (020) 4242000/
Wavuti: www.ca.go.ke

Zabuni zitafunguliwa mara moja baada ya hapo katika CA Centre, ghorofa ya chini, Atrium, mbele ya wawakilishi wa wazabuni wanaochagua kuhudhuria.

Head Office	Western Regional Office	Coast Regional Office	Central Regional Office	Nyanza Regional Office
CA Centre P.O.Box 14448 Nairobi 00800 Mobile: 0703042000 Email: info@ca.go.ke	1 st Floor KVDA Plaza P.O.Box 2346 Eldoret 30100 Mobile: 0703042105 Email: wro@ca.go.ke	3 rd Floor, NSSF Building P.O.Box 8041 Mombasa 80100 Mobile: 0703042152 Email: cro@ca.go.ke	Ground Floor, Advocates Plaza P.O Box 134 Nyeri 10100 Mobile: 0703042181 Email: cero@ca.go.ke	2 nd Floor Lake Basin Mall, P.O Box 2016 Kisumu 40100 Mobile: 0703042130 Email: nro@ca.go.ke



AGRICULTURE AND FOOD AUTHORITY (AFA)




NOTISI YA USHIRIKISHAJI WA UMMA

**UTHIBITISHAJI WA WASHIRIKI KWA MPANGO WA MKAKATI WA MWONGOZO
WA MAMLAKA YA KILIMO NA CHAKULA KWA MIAKA 2023-2027**


Mamlaka ya Kilimo na Chakula (AFA) ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo iliyoanzishwa na Sheria ya AFA Na. 13 ya 2013 ili kuendesha Sheria ya Mazao Na. 16 ya 2013. Majukumu ya Mamlaka ni kukuza na kudhibiti minyororo ya thamani ya mazao ya wakati uliopangwa ili kuongeza ukuaji wa kiuchumi nchini Kenya.


Kulingana na Ibara 10(2)(a) ya Katiba ya Kenya, Mamlaka kupitia taarifa hii inawaalika wadau wa sekta ya kilimo na umma kutoa maoni yao kuhusu Rasimu ya Mpango Mkakati wa Mamlaka kwa miaka 2023-2027.

Rasimu ya Mpango Mkakati wa Mamlaka kwa miaka 2023-2027 inapatikana kwa kupakuliwa kwenye tovuti ya AFA na inaweza kupatikana kupitia kiungo hiki: www.afa.go.ke au kupitia Nambari ya QR ifuatayo. Maoni na maswali zaidi yanaweza kutumwa kwa Mamlaka kupitia planning@afa.go.ke ifikapo tarehe 24 Oktoba 2023



Willis Audi
Mkurugenzi Mkuu





An ISO 9001:2015 Certified Hospital

MOI TEACHING AND REFERRAL HOSPITAL

OPEN NATIONAL TENDER

Moi Teaching and Referral Hospital (MTRH) invites sealed bids from eligible candidates for the under listed tenders.

NO	TENDER NO.	TENDER DESCRIPTION	ELIGIBILITY	CLOSING DATE
1	MTRH/T/42/2023-2026	Tender For Supply and Delivery of Dressing Items (Framework Contract)	Open Tender	17.11.2023
2	MTRH/T/44/2023-2026	Tender For Provision of Service of Vacuum Plant (Framework Contract)	Open Tender	17.11.2023
3	MTRH/T/47/2023-2024	Proposed Construction of ShoeAfrica Idella Rome Consultants' House at MTRH	Open Tender	17.11.2023
4	MTRH/T/50/2023-2024	Tender for Improvement of Drainage at Warehouse Building and AMPATH Basement.	Open Tender	17.11.2023
5	MTRH/T/51/2023-2024	Tender for Supply, Delivery and Installation of Cathlab Lead Doors and Lead Glass viewing window in Moi Teaching and Referral Hospital	Open Tender	17.11.2023

The eligible bidder shall be required to provide authenticated evidence that they have recently satisfactorily carried out similar assignment.

Notice of the advertisement will be in MTRH website and Public Procurement Information Portal. Tender document with detailed specifications can also be downloaded FREE OF CHARGE from both Hospital's website www.mtrh.go.ke or www.tenders.go.ke under tender portals.


Completed tender documents in plain sealed envelopes should be deposited in tender box number "A" located at Ground floor left wing of Chandaria Cancer and Chronic Diseases Centre (CCDC) Building of MTRH (Eldoret) or posted to:

**Chief Executive Officer
Moi Teaching and Referral Hospital
P.O. Box 3-30100
ELDORET**

So as to be received on or before **17th November, 2023** as indicated above at 10.00 a.m. Opening of the bidding documents will be conducted publicly immediately thereafter at a venue to be advised by Tender Opening Committee.

CHIEF EXECUTIVE OFFICER.

MOI TEACHING AND REFERRAL HOSPITAL

NATIONAL YOUTH SERVICE

TENDER NOTICE

**TENDER INVITATION NOTICE FOR THE PROPOSED
REHABILITATION OF SEWERAGE WORKS AT
NYS PARAMILITARY ACADEMY, NAKURU COUNTY
W.P ITEM NO. D1214/RV/NKU/2301 JOB NO. 1230A**

TENDER NO. NYS/ ONT / GILGIL/ 032 /2023-2024

The **NATIONAL YOUTH SERVICE (NYS)** invites sealed bids from eligible bidders for the proposed rehabilitation works on the sewer line at NYS Gilgil, Nakuru County.

A complete set of tender documents may be downloaded from the Service website: www.nys.go.ke or from the National Treasury Portal: www.tenders.go.ke **free of charge**. Tender documents may also be inspected and obtained in person, or against written application from the Supply Chain Management Office, located on first floor NYS Headquarters, Ruaraka upon payment of a non-refundable fee of Ksh.1, 000 paid in cash or bankers' cheque at the cash office, during official working hours between 9:00am- 4:00pm from Monday to Friday.

Prices quoted should be net inclusive of all taxes, must be in Kenya Shillings and shall remain valid for (120) days from the closing date of the tender. Bidders are required to provide Tender security equivalent of Five Hundred Thousand Shillings [Kshs. 500,000.00], which shall remain valid for 150 days from the date of Tender opening.


There shall be a pre-tender site visit at NYS Paramilitary Academy in Gilgil- Nakuru County on **Monday 23rd October 2023** starting at **11:00 am** for all prospective bidders to familiarize themselves with the project site conditions and topography.


Completed tender documents are to be enclosed in a plain sealed envelope marked with the tender number and be deposited in the Tender Box at the NYS Headquarters, Ruaraka, 1st floor so as to be received on or before **2nd November 2023 at 11.00 a.m.** and addressed to:

**THE DIRECTOR GENERAL/CEO
NATIONAL YOUTH SERVICE HEADQUARTERS
P. O. Box 30397-00100 NAIROBI.**

Tenders received will be opened immediately thereafter in the presence of Tenderers or their representatives who choose to attend at NYS Headquarters, Ruaraka.

**HEAD SUPPLY CHAIN MANAGEMENT SERVICES
FOR: DIRECTOR GENERAL**





KENYA REINSURANCE CORPORATION LIMITED

INVITATION TO TENDER

Kenya Reinsurance Corporation Limited invites sealed tenders from eligible candidates for the following item as detailed in the tender document:

TENDER NO.	DESCRIPTION	TENDER SECURITY (KSHS.)	TENDER SUBMISSION FORMAT	ELIGIBILITY
KRC/2023/2095/292	PROVISION OF SECURITY GUARDING SERVICES FOR KENYA RE COMMERCIAL BUILDINGS FOR YEAR 2023-2025	750,000.00 (for class A) 200,000.00 (for class B)	COMBINED FINANCIAL AND TECHNICAL	OPEN

Prospective bidders may download the tender documents from the Kenya Reinsurance Corporation Limited website www.kenyare.co.ke **free of charge** or Public Procurement Portal www.tenders.go.ke. Tender documents in plain sealed envelopes clearly bearing the correct tender number and name should be deposited in the Tender Box located on the **16th floor of Reinsurance Plaza Aga Khan Walk NAIROBI** or be sent to:-


**Managing Director
Kenya Reinsurance Corporation Limited
Reinsurance Plaza, Nairobi
Aga Khan Walk
P.O. Box 30271 - 00100 NAIROBI**

To be received before or on **31ST OCTOBER 2023 at 10.00 a.m.** as detailed in the invitation to tender. Tenders will be opened the same day and time in the Corporation's Boardroom in the presence of bidders or their representative who choose to attend. Tenders that are delivered after the submission deadline will be rejected.



Prices quoted **MUST** be expressed in Kenya Shillings as detailed in the invitation to tender inclusive of Kenyan Government taxes (**VAT, WITHHOLDING TAX**) and should remain valid for a period of **120 days** from the date of closing of the tender.

Bidders who download the tender documents from the Corporation website or the Public Procurement Portal **MUST** forward their particulars immediately via email to procurement@kenyare.co.ke. This is for record and any further tender clarifications and addendum where necessary. The particulars should include: Name of Firm, Postal Address, Telephone Number, Email Address, Tender Number and Tender Name. The said e-mail may be used for clarification.

Any canvassing or giving of false information will lead to automatic disqualification.



Kenya Re is ISO 9001:2015 and ISO 27001:2013 Certified



National Environment Management Authority

Popo Road, off Mombasa Road P.O.BOX 67839-00200, Nairobi, Kenya,
Tel: 0724253398, 0735013046 E-mail: dgnema@nema.go.ke Website: www.nema.go.ke

NOTISI KWA UMMA KUTOA MAONI KUHUSU RIPOTI YA TATHMINI YA MAZINGIRA YA MKAKATI KWA SERA YA USAFIRI YA KITAIFA ILIYOREKEBISHWA (INTP)

Kwa kuzingatia vifungu vya sehemu ya 57A ya Sheria ya Usimamizi na Ushirikiano wa Mazingira (EMCA) ya mwaka 1999, Kanuni ya 42 na 43 za Kanuni za Tathmini ya Athari za Mazingira na Ukaguzi wa Mazingira ya mwaka 2003, Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA) imepokea Ripoti ya Tathmini ya Mazingira ya Mkakati kwa Sera ya Usafiri ya Kitaifa iliyorekebisha (INTP). Matokeo ya Tathmini ya Mazingira ya Mkakati yanatarajiwa kuingiza sera, mipango, na programu za sekta zilizoopo ili kuanzisha njia za maendeleo endelevu.

Idara ya Usafiri ndiyo mwenye sera na inatambua kuwa INTP sahihi ndio nguzo ya kufikia mfumo bora wa usafiri unaokidhi mahitaji ya watu na sekta. INTP inakusudia kuchochea maendeleo ya nchi katika suala la kuunganisha vituo vya uzalishaji, masoko, na watu, hivyo kuwezesha usafirishaji katika maeneo ya vijijini na mijini, kuimarisha ushirikiano wa kitaifa na kikanda, kukuza biashara, kuboresha ustawi wa watu, na ushindani wa Kenya.

Sera hii inategemea kutambua kwamba, ujenzi wa miundombinu ya usafiri na matengenezo yake mara nyingi huathiri mazingira, husababisha kuhamishwa kwa makazi ya binadamu, upotevu wa maisha, mgawanyiko wa makazi kati ya mambo mengine mabadiliko mabaya katika mazingira. Kwa hivyo, kuna haja ya kuhakikisha kuwa masuala ya mazingira, kijamii, afya, na usalama yanajumuishwa katika maendeleo ya miundombinu ya usafiri, usimamizi, na uendeshaji ili kulinda mazingira na afya ya binadamu.

Muhtasari wa mpango wa usimamizi wa mazingira na ufuatiliaji uliopendekezwa kwa Sera ya Usafiri wa Kitaifa iliyoundwa kwenye jedwali hapa chini. Mikakati ya kupunguza athari zinakusudia kupunguza athari hasi wakati wa kuimarisha zile chanya.

Athari muhimu za Mazingira, Kijamii, Afya kazini na Usalama na Hatua za Kupunguza kwa INTP

MASUALA YA KIMAZINGIRA		
Suala	Hatua za Kupunguza	Kufuatilia
Uchafuzi (Hewa, Maji, Kelele)	<ul style="list-style-type: none"> Sera ya NEMA kuhusu kelele, viwango vya ubora wa hewa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Mazingira na Maliasili (Marekebisha ya 2006) Sheria ya Usalama na Afya Kazini, 2007 Sheria ya Afya ya Umma (Kifungu 242) Sheria ya Anga ya Raia, No. 21 ya 2013, Sheria ya Anga ya Raia (Marekebisha) No. 46 ya 2016, Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Kenya (KAA) Kifungu cha 395, cha 1991 na kanuni mbalimbali zinazohusiana na maeneo tofauti. Shirika la Kimataifa la Anga ya Raia (ICAO) Mkataba juu ya Aina ya Biolojia Duniani Mkataba wa Ramsar Mkataba kuhusu Aina za Wanyamapori Wanaohama/Bonn Convention Mkataba wa Bamako juu ya Kupiga Marufuku Uingizaji wa Taka Hatari Barani Afrika na Udhhibiti wa Usafirishaji wa Taka Hatari kuvuka Mipaka Barani Afrika (1997) Mkataba kuhusu Persistent Organic Pollutant (2001) 	Tathmini miongozo kuhusu mpango wa hatua katika sekta ya usafiri
Taka hatari	<ul style="list-style-type: none"> Kuzingatia/Ufuatiliaji/Ukubaliano/Ukaguzi kwa: Sheria ya Usimamizi Endelevu wa Taka ya 2022 Mkataba wa Bamako kuhusu Kupiga Marufuku Uingizaji wa Taka Hatari Barani Afrika na Udhhibiti wa Usafirishaji wa Taka Hatari kuvuka Mipaka Barani Afrika (1997) 	Tathmini miongozo kuhusu usimamizi wa taka.
Upotevu na uharibifu wa maeneo ya maji.	<ul style="list-style-type: none"> Kuzingatia/Ufuatiliaji/Ukubaliano kwa: Sheria ya Usimamizi Endelevu wa Taka ya 2022 Sheria ya Mabadiliko ya Tabianchi No. 11 ya 2016 Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mfumo wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) Sera ya Kitaifa ya Rasimu kuhusu Uhifadhi na Usimamizi wa Maeneo ya Maji (2013) Mkataba wa Ramsar Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyamapori ya 2013 Sera ya Mazingira ya Kitaifa, 2013 	Refusha miongozo kuhusu usimamizi wa maeneo ya upokeaji maji.
Uharibifu wa mimea na wanyama	<ul style="list-style-type: none"> Kuzingatia/Ufuatiliaji/Ukubaliano kwa: Mkataba wa Aina tofauti za Biolojia (IC/A/P) Mkataba juu ya Aina za Wanyamapori Wanaohama/Bonn Convention (IC/A/P) Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyamapori ya 2013 Sheria ya Misitu ya 2012 Sheria ya Usimamizi na Ushirikiano wa Mazingira ya 2015 (CAP 387) na Marekebisha yake Mkataba wa Lusaka kuhusu Operesheni za Utekelezaji wa Ushirikiano Didi ya Biashara Haramu ya Wanyama wa Pori (1994) 	Tathmini miongozo kuhusu usimamizi wa mimea na wanyama porini.
